UNIVERSITY OF BIRMINGHAM | THE INSTITUTE FOR GLOBAL INNOVATION

# ENGAGE

ENSURE NO 'GRAB AND GO' EXTRACTIVE RESEARCH

## Miongozo bora ya utenda kazi kuhusiana na dhuluma za kijinsia katika mataifa yenye kipato cha chini na kipato cha kati

GCRF
Global Challenges Research Fund

**Mradi wa HUSISHA (ENGAGE[1]) ni ushirikiano baina ya washiriki kutoka mataifa yenye kipato cha chini na kipato cha kati wakiwemo watafiti walio na uhusiano na Chuo Kikuu cha Birmingham iliyoko nchini Uingera. Ushirikiano yetu inajumuisha watu wanao fanya kazi kuhusiana na masuala za kijinsia na kuwasaidia waathiriwa wa dhuluma za kijinsia kutoka mataifa ya Guatemala, Kenya na Uganda – Timu ya Uingereza inawajumumisha wasomi kutoka Ulaya pamoja na washika dau wengine kutoka nyanja vitatu tofauti vya uuguzi, maendeleo na kazi za kijamii – ambao wote pia wana ujuzi kama wafanyi kazi na watafiti katika nyanja ya dhuluma za kijinsia na/au utafiti ya kuhusisha watu katika mataifa yenye yenye kipato cha chini na kipato cha kati.**

**Timu:** Caroline Bradbury-Jones[2], Brisna Caxaj[3], Wangu Kanja[4], Margaret Kyemba Kulaba[5], Nicole Robinson-Edwards[2], Siân Thomas[2] and Sanne Weber[2].

[1] HUSISHA ni tafsiri la neno la kiingera 'ENGAGE', ambalo pia ni jina halisi na kichwa na miongozo wa mradi huu. ENGAGE ni kifupisho la: 'Hakikisha Hakuna Utafiti wa Kunyakua na Kwenda na wa Kiuvumbuzi

[2] Chuo Kikuu Cha Birmingham, Uingereza
[3] Impunity Watch, Guatemala
[4] Wangu Kanja Foundation, Kenya
[5] ADOVIC, Uganda

# TATIZO

Dhuluma za kijinsia, ikiwemo dhuluma za kingono, ni mojawapo ya madhara hatari yanayo sababishwa na ukosefu wa usawa wa kijinsia. Japo yanafanyika ulimwenguni kote, waathiriwa kutoka mataifa yenye kipato cha chini na cha kati kwa kawaida huwa wanakabiliwa na shida maalum, hii ni kutokana na serikali kutoweka mikakati yakutosha kukabiliana na udhalimu, na kwa sababu ya kanuni yanayotokana na utamaduni au dini ambazo kwa kawaida huwalaumu waathiriwa baada ya wao kupitia dhuluma, hali hii husababisha unyanyapaa au kutengwa ama hata kutelekezwa. Kutokana na hali hii, dhuluma za kijinsia yana madhara za kimwili, hisia, kijamii na pia za kiuchumi.

Utafiti inamanufaa zaidi kwa sababu inafanya watu kuelewa sababu na madhara ya dhuluma za kijinsia, ikiwemo hali halisi ya wale ambao wamepitia dhuluma hizo. Kuelewa kule ni muhimu ilikubuni hatua pamoja na sera za kumaliza aina zote za dhuluma za kijinsia. Hali hii imefanya nyanja ya dhuluma za kijinsia kuwa kitengo muhimu cha utafiti, ikiangaziwa hasa sana na wasomi na watafiti kutoka mashirika za kijamii.

Ni muhimu kuelewa kuwa, utafiti kuhusu dhuluma za kijinsia haikosi changa moto. Kushiriki katika utafiti yanaweza kusababisha waathiriwa kupitia dhuluma tena, kutokana na kukumbuka machungu waliyopitia. Pia inaweza kuwaweka waathiriwa hatarini, hasa ikiwa wale waliyowadhulumu wangali karibu nao. Washiriki pia wanaweza kuwa hatarini kupitia unyanyapaa na hata kutengwa kutoka jamii zao ikiwa kuhusika kwao kutajulikana.

Matatizo haya huwa bayana hasa sana ikiwa utafiti itafanywa kwenye mataifa yenye kipato cha chini na kipato cha kati na watafiti kutoka mataifa za kigeni, kwa vile hii huleta hali ya kutokua na usawa na uwezo kati ya watafiti na washiriki na huenda ikasababisha kutoelewa kikamilifu mazingira na changa moto wanaopitia washiriki. Utafiti ni lazima itekelezwe kwa uangalifu, sio tu kuzuia kiwewe kwa mara nyingine kwa washiriki, bali pia kuhakisha matokeo mazuri katika hali na maisha ya wahusika pamoja na jamii wanamoishi. Ni muhimu kuhakikisha ya kwamba mbinu za kutekeleza utafiti zinabuniwa kwa uangalifu.

# TAARIFA YA MSINGI

Changamoto hili ndio ulikua mwanzo wa mradi ulioongozwa na Chuo Kikuu cha Birmingham na kufadhiliwa kupitia taasisi ya ubunifu ulimwenguni (Institute for Global Innovation) na hazina ya ulimwengu ya changamoto za utafiti (Global Challenges Research Fund). Utafiti wa mradi wa HUSISHA (ENGAGE) ilichangia katika kutengeneza miongozo hizi zinazotumika kwa sasa. Watafiti wote wanao husika katika mradi huu wako na ujuzi wa kufanya utafiti katika mataifa yenye kipato cha chini na kati. Kando na hayo wote walikuwa wametambua umuhimu wa kufanya utafiti kwa kutumia mbinu za kisasa kama vile utafiti wa kuhusisha na kutumia ubunifu. Mbinu za utafiti ya kuhusisha inatoa nafasi ya kufanya utafiti inayozuia unyanyasaji kwa mara nyingine kwa wahusika, kwa kuwahakikishia udhibiti wa shughuli hiyo kikamilifu. Inazingatia maadili na ushirikiano katika utafiti, huku ikihakikisha ya kuwa wahusika wanaweza kutengeneza na kudumisha umiliki wa maarifa yanayotokana na utafiti.

Mradi wa HUSISHA (ENGAGE) ilituwezesha kuelewa kiwango ambacho kuhusisha, ushirikiano na mbinu za ubunifu zinavyotumika kwa utafiti kuhusu dhuluma za kijinsia katika mataifa yenye kipato cha chini na cha kati. Tulifanya hayo mawili kupitia upimaji wa uhakiki, na kuchunguza aina tofauti ya na ukosefu kwenye mapendekezo ya mbinu bora ya matumizi ya ushiriki na ubunifu katika utafiti wa dhuluma za kijinsia katika mataifa wa kusini mwa ulimwengu, pia kwa kuchunguza kwa kina hali kulingana na kufanya utafiti kuhusu dhuluma za kijinsia katika mataifa yenye kipato cha chini na cha kati, kupitia mahojiano na mashirika ya uma na watafiti nchini Kenya, na pia kupitia warsha na washirika kutoka Uingera na wa kimataifa. Kutokana na hayo, tuliweza kutengeneza miongozo vya kisasa, na ni tumaini letu ya kuwa yatachangia katika kuweka kiwango cha kimataifa cha kufanya uchunguzi inayohusisha waathiriwa wa dhuluma za kijinsia katika nchi yenye kipato cha chini na kipato cha kati.

**Kwa maelezo zaidi, tafadhali tuma barua pepe:**
**c.bradbury-jones@bham.ac.uk**

# MIONGOZO

Miongozo ya sasa yamegawanywa kwa sehemu tatu tofauti, na kila moja inashughulikia suala muhimu kuhusiana na uundaji wa utafiti kuhusu dhuluma za kijinsia katika mataifa yenye kipato cha chini na cha kati. Zinajumuisha kanuni za mradi wa HUSISHA (ENGAGE), ambazo zinabainisha masuala za kimsingi za kuzingatiwa wakati wa kufanya utafiti kama huo na ambayo inapaswa kupeana mwongozo wakati wa kutengeneza taarifa ya nia ambayo washirika wote wa utafiti (Watafiti kutoka kaskazini mwa ulimwengu na watafiti kutoka nchi yenye kipato cha chini na cha kati, na washiriki) lazima watie sahihi kabla ya kuanzishwa kwa mradi yoyote wa utafiti. Yanajumuisha mfumo ya kuhakikisha waathiriwa wanaangaziwa, na kuuliza maswali muhimu, ilikuangalia kama kweli mradi wako wa utafiti inawapa waathiriwa kipaumbele na kuwahakikishia usalama, na hali njema. Hali hii inaweza kusaidia watafiti kuepukana na utafiti wa kinyonyaji (utafiti usio na manufaa kwa washiriki) na badala yake kuufanya lengo la kufanya utafiti kuwa wa maana na yenye kuleta mabadiliko endelevu kwa washiriki na wakati huo huo inachangia katika juhudi za kumaliza dhuluma za kijinsia ulimwenguni kote. Pia yanajumuisha mapendekezo ya masuala ya kimsingi yanayopaswa kujumuishwa katika mpango wa utafiti.

## Jinsi ya kutumia miongozo

Tumetengeneza miongozo kama njia mojawapo ya kuhakikisha ya kwamba utafiti kuhusu dhuluma za kijinsia katika mataifa yenye kipato cha chini na kipato cha kati inafanyika kwa njia bora, salama na inayozingatia maadili mema. Ikiwa haya yatazingatiwa, basi utafiti itakua ya yenye kuleta mabadiliko kwa wahusika wote. Ni muhimu kuelewa kuwa, utekelezaji wa miongozo hizi itatofautiana kutoka sehemu moja hadi nyingine.

Jedwali 1: Kutumia miongozo za HUSISHA (ENGAGE)

| NANI | JINSI GANI | WA NINI |
|---|---|---|
| **Washirika Kutoka mashikrika yasiyo ya kiserikali kutoka katika mataifa yenye kipato cha chini na kipato cha kati, vikundi vyao na waathiriwa wanaofanya kazi nao** | Kutumika ilikuelewa matarajio kutokana na utafiti hasa sana kuhusu majukumu, mchango na manufaa. | Wakati mwingine washirika Kutoka mashikrika yasiyo ya kiserikali pamoja na wale wanaosaidia (ikijumuisha waathiriwa wa dhuluma za kinjisia) huwa hawaelewi haki zao kulingana na utafiti. Wakati mwingine huwa wanahisi kana kwamba wanalazimishwa ilikuwezesha ushiriki wa jamii kwa njia isiyo ya manufaa kwao na hii huwa yana madhara yake. |
| **Watafiti wanaochunguza dhuluma za kinjisia katika mataifa yenye kipato cha chini na cha kati** | Kutumika ilikuelewa matarajio kutokana na utafiti, yapi ya kujadiliana na wafadhili au washirika wa kimataifa na jinisi ya kuwalinda washiriki. | Wakati mwingine watafiti kutoka katika mataifa yenye kipato cha chini na kipato cha kati huwa wanahisi kushinikizwa ilikuwezesha shughuli za utafiti kama vile usajili wa washiriki wasiofaa au salama. Wakati mwingine huwa wanaachwa nje kwenye awamu muhimu ya utafiti kama vile kudhanisha, matokeo ya utafiti na hata machapisho. |
| **Watafiti Kutoka kaskazini mwa ulimwengu (Mataifa za Kigeni)** | Kama mfumo wa kuhakikisha usawa na usalama katika utenda kazi. Yakutumika na washirika wa kitaaluma na wa kutoka mashirika yasiyo ya kiserikali kutoka mataifa yenye kipato cha chini na cha kati ili waweze kutambua haki zao katika utafiti wa kuhusu dhuluma za kijinsia na wanadhihirisha kujitolea kwao kulingana na mwongozo wa mradi wa HUSISHA (ENGAGE). | Ni muhimu kutunga kanuni za utenda kazi kulingana na miongozo ya mradi wa HUSISHA (ENGAGE). Kuyasambaza mapema inakuza na kuimarisha uaminifu katika mchakato ya utafiti, na inaweza kuufanya utafiti uwe yenye kuleta mabadiliko endelevu kwa waathiriwa wa dhuluma za kijinsia na kuweka dhana ya utafiti kwa pamoja. |
| **Dhuluma za Kijinsia na Watungaji wa sera za utafiti** | Kuwezesha uundaji wa sera kuhusu utenda kazi bora katika utafiti wa dhuluma za kijinsia kutoka mataifa yenye kipato cha chini na cha kati na kuhakikisha ya kwamba utafiti inazingatia viwango vinavyohitajika vya maadili. | Kuna hatari ya sera kukinzana kuhusu kushughulikia dhuluma za kijinsia na utafiti katika mataifa yenye kipato cha chini na cha kati. Miongozo ya HUSISHA (ENGAGE) inaleta yote mawili pamoja. |

## UNYETI

Washirika wote wanaohusika ni lazima wayaangazie asili nyeti ya mada ya utafiti na umuhimu wake maeneo ya mashinani.

## USHIRIKIANO

Washirika wanaotoka eneo ambalo utafiti unapaswa kutekelezwa, ni lazima wahusishwe kwenye hatua zote za utafiti, ikiwemo wakati wa kutunga swala la utafiti, kubuni mbinu, ukusanyaji, usindikaji na uchambuzi wa takwimu na utengenezaji wa matokeo (yawe ya kitaaluma au hata za kisera).

## VIGEZO VINAVYOWEZA KUTOKEA

Watafiti wanapaswa kuwa tayari kukabiliana na vigezo vinavyoweza kutokea wakati wa kutekeleza mradi wa utafiti na sharti wayajadili haya kwa uwazi na washirika wa eneo hilo. Vigezo kama hivi vinaweza kua, washiriki katika utafiti kuhisi kutowezeshwa, kutumiwa vibaya au kufadhaishwa. Zaidi ya kutarajia vigezo hivi, washirika wote ni sharti wajiandae na njia mwafaka ilikuyashughulikia shida hizo zinapoibuka: kwa mfano kuwapa waathiriwa usaidizi za kisaikolojia.

## MANUFAA KWA WASHIRIKA

Washirika wanaotoka eneo ambalo utafiti unapaswa kutekelezwa, ni lazima wahusishwe tangu mwanzo wa mradi huku muda wa kutosha wa kujenga mahusiano ikizingatiwa, kujadili mada na kukubaliana juu ya matokeo ya utafiti. Ni sharti pawe na makubaliano kuhusu muda wa kutekeleza mwanzoni wa mradi.

# KANUNI ZA HUSISHA (ENGAGE)

Kanuni za HUSISHA (ENGAGE) zinaorodhesha masuala muhimu ambayo watafiti wanapaswa kuzingatia wakati wa kufanya mradi wa utafiti ili kuhakikisha kuwa utafiti unaepuka kuwadhuru washiriki na badala yake inakusudia kuleta mabadiliko kutokana na hali ya waathiriwa wa dhuluma za kijinsia. Hatua ya kwanza ni kufahamu na kuelewa **unyeti** wa asili ya utafiti na **vigezo zinazoweza kujitokeza** kwa washiriki wa utafiti ikiwa ni pamoja na unyanyapaa. Hizi zinaweza kuwa masuala maalum kuhusiana na eneo fulani, kwani tofauti za kitamaduni na kidini unaweza kuleta changamoto na kusababisha hatari tofauti (ikiwemo za kisheria) kwa watafiti na washiriki. Kuchambua na kuyakisia hatari hizi ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa utafiti hautaweka washiriki katika hali ya hatari. Uchambuzi wa vigezo unapaswa kufanywa kwa njia ya **ushirikiano**, kwani washiriki mara nyingi huwa wanaelewa hatari za kiusalama vinavyowakabili. Wadau wote katika mchakato wa utafiti (wakiwemo waathiriwa wa dhuluma za kijinsia, watafiti wa kitaifa na kimataifa) lazima wawe na fursa ya kutambua kile wanachokiona kama **manufaa zinazoweza kutokea** kuhusiana na utafiti, kuanzia machapisho, kushawishi au shughuli za jamii.

Wanapaswa pia kujadili peupe na kwa uwazi jinsi kila mmoja wao anaweza kuchangia kuafikia malengo haya, hii ni pamoja na kuweka malengo na matarajio yanayoweza kuafikiwa. Kwa kufanya hivi, wahusika wote katika mchakato wa utafiti watahisi maoni yao yanapewa thamani sawa, na wataelewa ni jinsi gani utafiti unaweza kuleta mabadiliko kwa hali yao ya kibinafsi na kutatua shida za kijamii ambao inawahusu. Hii itasaidia kuepushana na shughuli za utafiti kuwa wa kinyonyaji au yenye kuwatumia vibaya washiriki.

**Masuala yote yaliyomo kwenye miongozo lazima yaangaziwe kwenye taarifa ya nia ambayo inapaswa kutiwa sahihi na wote wanaohusika katika utafiti mwanzoni mwa mradi.**

# MFUMO INAYOWAPA WAATHIRIWA KIPAUMBELE

Mfumo wa HUSISHA (ENGAGE) unaowaangazia waathiriwa wa dhuluma za kijinsia kwa utafiti inayaweka wazi masuala muhimu za utenda kazi, ili kuwaongoza makundi mbali mbali katika kubuni miradi inayohusisha na kuangalia ikiwa miradi yanazingatia na kuweka usalama, hali na sauti ya waathiriwa mbele katika mchakato nzima ya utafiti. Mfumo huu umepangwa kwa vitengo vinne vifuatavyo: **1) Eneo:** Inakusudia kuelewa eneo au mazingira hasa kuhusiana na kisiasa, kihistoria na kijamii, na hii ina maana gani kulingana na hali pamoja na vile dhuluma za kijinsia zinavyoeleweka; **2) Mahusiano:** Inakusudia kuhakikisha kuwa tunaunda ushirikiano wa kweli kati ya washirika wote, ambao unatambua michango na unanufaisha wote; **3) Kutafakari:** Inakusudia kuchunguza uhakiki wa mada ya utafiti, jinsi tunavyofanya kazi pamoja, na pia jinsi tunaweza kutafakari kuhusu maadili na mawazo ambayo sote tunaleta kwenye mchakato wa utafiti; na **4) Mabadiliko Endelevu:** Inakusudia kuelewa jinsi ya kuleta mabadiliko mema ya kijamii kupitia mchakato na matokeo ya utafiti ili iweze kunufaisha waathiriwa na jamii nzima.

Kutilia mkazo, vitengo vyote vinne ni sharti yaambatane na mbinu ya kuhakikisha ya kwamba waathiriwa wa dhuluma za kijinsia wana pewa kipaumbele, usalama na ushiriki ambazo ni nguzo muhimu katika mchakato wa utafiti. Maswali yanakusudiwa kutumiwa kwa ushirikiano na washirika wote kwenye mradi, kama njia ya kuchunguza na kujadili utofauti wa matarajio, uelewa na utaalamu baina ya washiriki na watafiti.

## TAFAKARI

**Tunayawazia vipi mambo?**

- Ni maadili na mawazo yapi tunayoleta:
  – Kwa mchakato wa utafiti?
  – Kwa uhusiano kati yetu?
- Ni michakato gani inayoweza kutusaidia kutafakari pamoja?

**Tutaleta aje mabadiliko?**

- Mabadiliko bora yatakua aje?
- Nani atakaye amua?
- Nani ana uwezo wa kuleta mabadiliko?
- Ni vipi tunaweza kuutekeleza? (sera, elimu, utetezi, mikakati, n.k)

## MABADILIKO ENDELEVU

## MBINU INAYOWAPA WAATHIRIWA KIPAUMBELE

## ENEO AU MAZINGIRA

**Ni nini tunajua kuhusu eneo au mazingira la kufanya utafiti?**

- Mazingira ya kisiasa, historia na kimila ikoje?
- Nani ana utalaamu?
- Eneo au mazingira itachangia vipi kuhusiana na vigezo, unyeti (mambo yanayopewa uzito) na kueleweka kwa masuala ya dhuluma za kijinsia?

## MAHUSIANO

**Tutaweza aje kufanya kazi pamoja?**

- Nani atashiriki?
- Nani ananufaika?
- Nani ana amua?
- Tutagawana aje majukumu?
- Tutahakikisha aje kuheshimiwa kwa tofauti zetu?
- Tutahakikisha aje uwakilishi halisi?
- Tunawezaje kudhibiti ukosefu wa usawa katika uwezo?

## MUDA

Mpango wa utafiti unahitaji muda unaofaa unaoruhusu uimarishaji na ushiriki wa maana katika awamu zote za utafiti.

## WATAFITI WENZA

Maendeleo ya pamoja na ya kweli ni sharti iwe lengo kuu, huku washirika wote wakifanya kazi kama watafiti wenza.

## MASUALA YA KIMAADILI

Mpango wa utafiti unapaswa kujihusisha na masuala ya kimaadili yanayoweza kuchipuza kutokana na mradi. Maadili ya kutekeleza utafiti inahitaji kufikiriwa kupitia mahusiano ama ushirika kwenye viwango viwili tofauti: na watafiti waliyo kwenye vyuo vikuu ama mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyomo mashinani na washiriki katika utafiti.

## MAWASILIANO

Mawasiliano bora yanapaswa kudumishwa baina ya washirika wote, ikiwemo watafiti kutoka mataifa yenye kipato cha chini na cha kati na ikiwezekana washiriki, wakati wa kutengenezwa kwa mpango wa utafiti.

abc

## LUGHA

Mpango wa utafiti ni sharti itengenezwe kwa lugha inayoeleweka na washiriki walio mashinani.

# MAMBO YA MSINGI KUHUSIANA NA MPANGO WA UTAFITI

Majadiliano ya pamoja na uchambuzi kulingana na kanuni za HUSISHA (ENGAGE) itawezesha ushirikiano na ufafanuzi na kuboreshwa kwa mpango wa utafiti. Mpango huu wa utafiti utaainisha na kuangazia hatua tofauti ambazo mchakato wa utafiti utajumuisha. Utakuwa na **wakati** halisi kwa kila awamu tofauti za utafiti: ukusanyaji wa takwimu, ikiwa ni pamoja na mbinu maalum ambazo zitatumika; uchambuzi wa takwimu; kuandika juu ya matokeo ya utafiti katika machapisho, na pia uwezekano wa uboreshaji katika awamu hizi tofauti. Kwa kila moja ya awamu hizi mpango huo utabaini jukumu la **watafiti wenza** tofauti, wakiwemo waathiriwa wa dhuluma za kijinsia. Ni muhimu pia kutambua majukumu ya washiriki na watafiti kutoka kwenye mataifa yenye kipato cha chini na cha kati kwenye chapisho ya matokeo ya utafiti, kwa sababu hii hatua huwa inatengewa washirika wa utafiti kutoka sekta ya elimu katika mradi wa utafiti. Matokeo mbalimbali ya utafiti yanapaswa kuzingatiwa, ikiwalenga watu tofauti na kwa madhumuni tofauti, kulingana na mahitaji na maoni ya watafiti wenza wote.

Kimsingi, mpango wa utafiti utaelezea **masuala ya kimaadili** ambayo watafiti-wenza wanakisia na hatua za kuzuia na kuepukana na vigezo hivo. Faragha, usiri na kutokujulikana ni masuala muhimu ya kushughulikia hapa, pamoja na uwezekano wa msaada wa kisaikolojia au aina nyingine ya msaada kwa waathiriwa wa dhuluma za kijinsia na watafiti. Mpango wa utafiti pia utaweka na kusisitiza makubaliano kuhusu **mawasiliano** kati ya watafiti wenza kulingana na wakati na aina ya mawasiliano, pamoja na jinsi migogoro (kutoelewana) yatajadiliwa na kutatuliwa. Inapaswa kutumia **lugha** inayoeleweka na kuepukana na maneno yanayoweza kutatanisha ili kuhakikisha mpango wa utafiti unaeleweka na ni muhimu kwa watafiti wenza wote. Hatimaye, mpango wa utafiti utasaidia katika ufafanuzi na kuboreshwa kwa **taarifa ya nia** ambayo pia itatilia mkazo mambo ya kimsingi ya mpango wa utafiti, na itatiwa sahihi na watafiti wenza wote. Taarifa hii ya nia huimarisha uwazi wa mchakato wa utafiti, husaidia kukuza uwajibikaji baina ya watafiti wenza wote na hivyo basi inakuza uaminifu kati yao.

**Masuala yote katika miongozo lazima yaangaziwe kwenye taarifa ya nia, ambayo inapaswa kutiwa sahihi na wote wanao husika katika utafiti mwanzoni wa mradi.**

# SHUKRANI

Shukrani kwa kushiriki katika kutengeneza miongozo ya HUSISHA (ENGAGE).

Timothy Atwine (Mtengeneza filamu wa kibinafsi)
Dkt. Heather Flowe (Chuo Kikuu cha Birmingham)
Josefina Grunwald (Mwanafunzi wa tarajali katika Chuo Kikuu cha Birmingham 2020)
Margaret Hardiman (Chuo Kikuu cha Birmingham)
Dkt. Louise Isham (Chuo Kikuu cha Birmingham)
Dkt. Laura Martin (Chuo Kikuu cha Sheffield)
Aurelia Munene (Eider Africa)
Sarah Rockowitz (Chuo Kikuu cha Birmingham)
Dana Sammut (Chuo Kikuu cha Birmingham)
Prof. Julie Taylor (Chuo Kikuu cha Birmingham)
Chi-chi Undie (Population Council)
Dkt Christalla Yakinthou (Chuo Kikuu cha Birmingham)

WANGU KANJA FOUNDATION

GCRF Global Challenges Research Fund

impunity watch

adovic Anti Domestic Violence Centre

UNIVERSITY OF BIRMINGHAM

THE INSTITUTE FOR GLOBAL INNOVATION

UNIVERSITY OF BIRMINGHAM

Edgbaston, Birmingham,
B15 2TT, United Kingdom
www.birmingham.ac.uk

Designed and printed by

UNIVERSITY OF BIRMINGHAM | creativemedia

21589 © University of Birmingham 2021.